**THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL**

# Gredi ya 8

# Mwongozo wa Kutathminia

# SEHEMU B na C

# SEPTEMBA 2024

**MWONGOZO HUU UNA KURASA 10 ZILIZOPIGWA CHAPA.**

**ZOEZI 3: KUSOMA KWA UFAHAMU**

1. Alikwenda sokoni kununua bidhaa za kutumia wiki nzima

**Hoja 1 x1 =1**

2. **Jukumu la mnunuzi:**
   i. Kuandaa orodha ya bidhaa atakazonunua.
   ii. Kununua bidhaa kulingana na orodha.
   iii. Kukadiria ubora wa bidhaa
   iv. Kukadiria bei ya bidhaa

**Hoja 1 x1 =1**

3. **Yafuatayo yangetokea:**
   i. Angesahau kununua bidhaa alizohitaji
   ii. Angenunua bidhaa asizohitaji.
   iii. Angetumia hela visivyo.
   iv. Huenda akananunua bidhaa moja mara mbili.
   v. Atakosa kukadiria matumizi ya pesa.

**Hoja 1 x1 =1**

4. **Maana ya akaridhia**
   i. Akakubaliana na wazo hilo.
   ii. Akatosheka

**Hoja 1x1 =1**

5. kumkinga Binadamu dhidi ya adui wa kila namna. **Hoja 1x1 = 1**
6. D. **Hoja 1x1 = 1**

7. **Matokeo ya urafiki kuisha:**
   i. Panya alihamia msituni
   ii. Binadamu alianza kumwinda Panya.
   iii. Binadamu alitafuta mlinzi mwingine.
   iv. Wadudu waharibifu waliongezeka ghalani.
   v. Hifadhi ya nafaka iliboreka.
   vi. Panya aliteseka kwa njaa.
   vii. Binadamu alianza kuvamiwa na wezi.
   viii. Binadamu alianza kuwa makini ziadi kuhusu marafiki.

**Hoja 1x1 =1**

8. A- analalamika **Hoja 1x1 =1**

**UFUPISHO**

9. Maana ya mto kwa maneno yasiyozidi sita
   i. Mto ni maji yanayofanya njia yake.
   ii. Mto ni mkondo wa maji yanayotiririka.
   iii. Mto ni maji yanayotoka sehemu ya juu hadi ya chini.

**Hoja 1x1= 1**

10. **Ufupisho wa kauli zilizokolezwa rangi katika aya ya kwanza.**
    i. Mito hutofautiana kwa kina, urefu, upana na kasi ya kutirirka  kwa maji.
    ii. Kina, urefu upana na kasi ya kutiririka  kwa maji ya mito ni tofauti.

**Hoja 1x1= 1**

11. **Umuhimu wa mito katika ukuzaji wa uchumi.**
    i. Mito huwezesha uzalishaji bora wa mazao ya shambani, usafirishaji, ubadilishanaji wa bidhaa na huduma.

**Hoja 1x1= 1**

12. **Ushauri wa mwandishi kwa maneno 6**
    i. Kila mwanajamii anapaswa kutunza mito
    ii. Sote tuwajibikie utunzaji wa mito
    iii. Utunzaji mito ni jukumu letu sote.

**Hoja 1x1= 1**

# ZOEZI 4: SARUFI

13. B (alama 1)
14. D (alama 1)
15. A (alama 1)
16. B ( alama 1)
17. C (alama 1)
18. mabivu – Kivumishi

    kesho- Kielezi

    (alama 2)
19. Koja alikuwa amepalilia shamba kwa jembe hili. (alama 2/0)
20. Wangu ni mwigizaji hodari (alama 2)

    Wake amechora picha nzuri

    Chenu kinapendeza

    **Tanbihi: Hakiki majibu.**
21. Jenga-Bomoa/ jengua

Kaza - legeza (alama 2)

22. Juma hakubuni kisa cha kusisimua. (alama 1)

23. Banda/ Jibanda limesafishwa. (alama 2/0)

24. Tumieni ujana wenu kwa faida ya jamii zenu. (alama 2/0)

25. Tamara alimwambia mwenzake amsomee aya hiyo ili atathmini jinsi alivyotamka/alivyokuwa akitamka. (alama 2)

**ZOEZI 5 : KUANDIKA (alama 10)**

26. Hii ni barua ya kirafiki ya kutoa shukrani.

Vitathminiwa vifuatavyo vishughulikiwe ;

i. Muundo

- Iwe na anwani ya mwandishi
- Mtajo : Kwa mzazi/mlezi mpendwa/ Mpendwa mama/ Mpendwa baba.
- Mwili : Pawe na utangulizi ambapo kiini barua kinabainishwa.
- Hitimisho : Kujumuisha hoja/ muhtasari na kuaga.
- Kimalizio cha heshima : Mimi mwanao mpendwa, Binti wako mpendwa.

ii. Mtindo

- Hoja kutengwa katika aya
- Uzungumzaji wa moja kwa moja
- Mtindo ni wa kimaelezo
- Matumizi ya lugha sanifu

iii. Maudhui

Hoja zifuatazo zinaweza kujitokeza :

- Kutoa shukrani
- Kubainisha pengo/ tatitizo lililokuwapo kabla ya kununuliwa
- Kueleza kinavyomnufaisha
- Barua ibainishe manufaa k.m kurahisisha ujifunzaji, kuhifadhi kazi yake, kukuza ujuzi wa kidijitali,
- Kumpunguzia aibu ya kuazima kila mara

- Kutoa ahadi ya kukitunza
- Kuzingatia usalama mtandaoni

**Tanbihi:**

i. Mwanafunzi ana uhuru wa kuzingatia masuala yoyote yanayohusiana na maudhui ya insha lengwa.
ii. Katika kutuza, mwalimu azingatie vigezo vifuatavyo ili kutathmini kiwango cha utendaji cha mwanafunzi. Viwango hivyo ni Kiwango cha 4, 3, 2 na 1
iii. Kiwango hicho ndicho atakachorekodi kwenye jedwali la alama.

**Viwango vya kutathminia**

| **Vigezo vya kutathminia** | **Kuzidi matarajio**<br>**4** | **Kufikia matarajio**<br>**3** | **Kukaribia matarajio**<br>**2** | **Mbali na matarajio**<br>**1** |
|---|---|---|---|---|
| Sarufi na ufundi wa uandishi | Anadhihirisha umilisi wa kiwango cha juu cha sarufi, uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wake. | Anatumia sarufi, alama za uakifishaji na kuendeleza maneno ipasavyo katika uandishi.<br>Hata hivyo, ana makosa machache ambayo hayatatizi usomaji. | Ana makosa ya sarufi, uakifishaji na maendelezo ya maneno ambayo yanatatiza usomaji wa sehemu za insha yake. | Ana makosa mengi ya sarufi, uakifishaji na maendelezo ya maneno kuanzia mwanzo hadi mwisho wa uandishi.<br>Msomaji anaweza tu kukisia maana. |
| Mwandiko | Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi.<br>Anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari.<br>Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno kutoka mwanzo hadi mwisho wa insha. | Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi.<br>Anatenganisha herufi nyingi ipasavyo.<br>Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno. | Ana mwandiko usio nadhifu lakini unasomeka.<br>Anatenganisha baadhi ya herufi ipasavyo.<br>Anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno. | Ana mwandiko usiosomeka kwa urahisi.<br>Hatenganishi herufi nyingi ipasavyo.<br>Anaacha nafasi nyingi zisizolingana baina ya maneno. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Msamiati | Ana uteuzi mzuri wa maneno na matumizi anuwai ya msamiati kulingana na muktadha. | Ana uteuzi mzuri wa msamiati uliotumika kulingana na muktadha. | Anatumia msamiati finyu ambao wakati mwingi haulingani na muktadha. | Anatumia msamiati finyu ambao haulingani na muktadha. |
| Mpangilio (Muundo na mtindo) | Ana uwiano na mpangilio wa kipekee wa mawazo kuanzia mwanzo hadi mwisho.<br>Amebainisha utangulizi, mwili na hitimisho vilivyo.<br>Anaendeleza mawazo vizuri. | Ana mtiririko wenye mantiki.<br>Kuna uwiano na mfululizo wa mawazo.<br>Kuna utangulizi, mwili na hitimisho.<br>Anaendeleza mawazo vizuri. | Anajaribu kupanga mawazo kimantiki.<br>Utangulizi, mwili na hitimisho hujitokeza kwa kiasi.<br>Anaendeleza baadhi ya mawazo vizuri. | Hana mpangilio unaoeleweka wa mawazo na ni vigumu kufuatilia kazi yake. |

## SEHEMU C : FASIHI

### ZOEZI 6: FASIHI SIMULIZI (alama 10)

27. **a. Ithibati ya hurafa**

i. Wahusika wanyama
ii. Wanyama wanatenda kama binadamu
iii. Wanyama kujisemea
iv. Kuwa na viganja

Hoja 2x1=2

b. **Ujumbe wa hadithi** (alama 2)

i. Matatizo yanayowakumba wanajamii/ wanyama
ii. Utatuzi wa matatizo/ jinsi ya kuyatatua
iii. Mahusiano ya kijamii- namna nyani walivyohusiana
- Fisi kuwa adui wa nyani

**c. Mbinu za lugha za kufanikisha uwasilishaji wa hadithi hii :**

**Tashbihi :** iliyokamata kama sumaku
Wakatetemeka utadhani ni jani wakati wa upepo mkali
Kujikaukia kama ukuni
**Nahau :** Mguu niponye
Alitivua kivumbi
**Chuku :** Ungecheka mbavu zivunjkie
**Urudiaji/ Takriri :** Walikimbia, wakakimbia, wakakimbia-a-a
**Uzungumzi nafsi :** laiti ingalikuwa kama mimi ?

(alama 2)

d. **Mbinu ya kuwasilisha:**

i. Nitaigiza
ii. Nitajitikisa/ nitatetemesha mwili,
iii. Nitashusha sauti.
iv. Nitajikunyata kuonyesha hofu.

(alama 2)

e. **Sifa za nyani aliyejificha shimoni** (alama 2)

i. **Mwenye kiburi-** laiti wangalikuwa kama mimi.
ii. **Mwenye busara**- anatoka shimoni anapoona ni salama.
iii. **Mwenye ubinafsi** - ninawahurumia

**28. ZOEZI 7 : TAMTHILIA (alama 10)**

**a) Masuala yanayozungumziwa katika sehemu hii ya tamthilia:**

- Changamoto za watu wenye mahitaji maalumu -Okilo kutembea kwa mikongojo.
- Uwajibikaji- serikali kuwasajili na kuwasaidia.
- Mshikamano wa kifamilia- Okilo kumsaidia mkewe kazi.
- Uraia- Watu wanatii sheria
- Maadili- Watu kutii sheria.
- Bidii- Mkewe Okilo ana bidii kazini.
- Ndoa- Okilo na mkewe kushirikiana

**(Hoja 2x1= 2)**

**b) Umuhimu mandhari (Hoja 2x1=2)**

- **Mahali**- nyumba ya msonge kuonyesha hali ya chini ya kiuchumi.
- **Hali-** Mzee Okilo anatumia mikongojo. Kuonyesha mgogoro/ tatizo linalokumba Okilo na wengine wa umbo lake.
- **Wakati-** Asubuhi/ macheo yanatujengea maudhui k.v uwajibikaji na sifa za wahusika kwa mfano bidii, sifa za mkewe Okilo, Chifu.

**c) Sifa za Okilo**

- Mwenye mlahaka mwema- anamkaribisha Chifu vyema.
- Mwenye kuwajibika- anamsaidia mkewe.
- Mcheshi- anaibua ucheshi katika mazungumzo yake na Chifu. K.m anaomba kwa ucheshi kuongezewa miwani.
- Mwadilifu-anatumai hakuna aliyevunja sheria kwake.
- Mwenye huruma- alimhurumia mkewe.
- Mwenye heshima- anajaribu kuinuka kumsalimia chifu.

**Hoja 3x1-3**

**Hakiki majibu ya mwanafunzi ipasavyo.**

d) **Mbinu za lugha zilizotumika katika dondoo :**

- **Tashbihi** –Mkawa weupe kama pamba
- **Tanakuzi/ kinyume-** akitoka anarudi, macheo /mafungia ng'ombe
- **Methali-** ajizi ni nyumba ya njaa.
- **Nahau-** akisafisha koo
- **Urudiaji-** papo hapo, ndipo..

**Hoja 3x1-3**

**MIPAKA YA KUTUZIA SEHEMU B NA C**

**ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA (READING COMPREHENSION)**

| UPEO/ALAMA (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 7-8 | 4 |
| 5-6 | 3 |
| 3-4 | 2 |
| 1-2 | 1 |

**ZOEZI 4: SARUFI (GRAMMAR)**

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| **16-20** | **4** |
| **11-15** | **3** |
| **6-10** | **2** |
| **1-5** | **1** |

**ZOEZI 5: KUANDIKA (WRITING)**

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 8-10 | 4 |
| 5-7 | 3 |
| 3-4 | 2 |
| 1-2 | 1 |

## SEHEMU C: FASIHI

### ZOEZI 6: FASIHI SIMULIZI (ORAL LITERATURE)

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 8-10 | 4 |
| 5-7 | 3 |
| 3-4 | 2 |
| 1-2 | 1 |
| **ZOEZI 7: TAMTHILIA** | |
| **UPEO (SCOPE)** | **KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS)** |
| 8-10 | 4 |
| 5-7 | 3 |
| 3-4 | 2 |
| 1-2 | 1 |

# KISWAHILI GRADE 8 ASSESSMENT SHEET: SEHEMU B

**(Tumia vigezo vya kutathminia ili kurekodi kiwango cha utendaji cha mwanafunzi: 4, 3, 2 ama 1)**

| | | ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA | | | | ZOEZI 4: SARUFI | | | | ZOEZI 5: KUANDIKA | | | | ZOEZI 6: FASIHI SIMULIZI | | | | ZOEZI 7: TAMTHILIA | | | | MAONI KUHUSU UTENDAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| NO | JINA LA MWANAFUNZI | 4 | 3 | 2 | 1 | 4 | 3 | 2 | 1 | 4 | 3 | 2 | 1 | 4 | 3 | 2 | 1 | 4 | 3 | 2 | 1 | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |